

JAMHURI YA MUUGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - TAMISEMI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU AJIRA YA WALIMU WA SAYANSI NA HISABATI NA MAFUNDI SANIFU MAABARA KWA SHULE ZA SEKONDARI - AWAMU YA PILI MWAKA, 2017

OR - TAMISEMI inapenda kuutarifu Umma kuwa, baada ya uhakiki wa maombi yaliyotumwa, jumla ya Walimu 381 na Mafundi Sanifu wa Maabara 137 wamechaguliwa na kupangiwa vituo vya kazi kwenye shule za Sekondari mbalimbali nchini. Walimu na Mafundi Sanifu wa Maabara waliopangiwa vituo vya kazi wanatakiwa kuripoti katika Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zilipo shule walizopangiwa na baadaye kwenye Shule walizopangiwa. Wote wanatakiwa kuripoti kuanzia tarehe 17 Julai, 2017 hadi tarehe 21 Julai, 2017 wakiwa na mahitaji yafuatayo:

- (i) Vyeti halisi vya taaluma vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita;
- (ii) Cheti halisi cha kitaalam cha kuhitimu mafunzo ya Ualimu katika ngazi husika; na
- (iii) Cheti cha kuzaliwa.

Walimu na Mafundi Sanifu wa Maabara wote wanaelekezwa kuwa:

- i. Vituo vyao vya kazi ni shule za Sekondari walizopangiwa na sio makao makuu ya Halmashauri.

- ii. Mwajiriwa atakayechukua posho ya kujikimu na baadaye kutoripoti na kuanza kazi katika kituo chake cha kazi alichopangiwa atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria.
- iii. Hakutakuwa na uhamisho ndani ya Mkoa au Halmashauri bila ridhaa ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Wakurugenzi wa Halmashauri wanatakiwa kuwapokea Walimu na Mafundi Sanifu wa Maabara kwa kuzingatia taratibu na kanuni zote za utumishi wa Umma ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya kuripoti kwao. Taarifa ya kuripoti waajiriwa hao itumwe Ofisi ya Rais- TAMISEMI ifikapo au kabla ya tarehe 25.07.2017 baada ya tarehe ya mwisho ya kuripoti.

Majina ya Walimu na Mafundi Sanifu Maabara waliopangiwa vituo yanapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI ya www.tamisemi.go.tz

Imetolewa na:
KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS - TAMISEMI